

4.0 KISWAHILI (102)

4.1 MATOKEO YA MTIHANI WA SOMO LA KISWAHILI

Jedwali hili linaonyesha matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili muda wa miaka minne (2005 hadi 2008).

Jedwali 6: Matokeo ya mtihani wa Kiswahili (2005 – 2008)

Mwaka	Karatasi	Watahiniwa	Alama ya Juu	Alama ya Wastani	Alama ya Tanganisho
2005	1	259,301	40	20.25	6.37
	2		80	34.08	10.61
	3		80	37.57	14.01
	Jumla	259,301	200	91.89	26.00
2006	1	241,272	40	15.31	7.68
	2		80	40.60	11.80
	3		80	48.48	14.63
	Jumla	241,272	200	104.39	29.00
2007	1	272,905	40	15.80	6.42
	2		80	32.22	11.91
	3		80	43.49	13.12
	Jumla	272,905	200	91.51	27.00
2008	1	304,314	40	14.20	7.18
	2		80	29.18	11.43
	3		80	31.17	13.64
	Jumla	304,314	200	74.55	32.25

Jedwali hili laonyesha kuwa:

- 4.1.1 Alama ya wastani ya ***karatasi ya 1(102/1)*** ya mwaka wa 2008 imeshuka ikilinganishwa na ya mwaka wa 2007.
- 4.1.2 Matokeo ya ***karatasi ya pili (102/2)*** ya mwaka wa 2008 yameshuka yakilinganishwa na ya mwaka wa 2007.
- 4.1.3 Vilevile, matokeo ya ***karatasi ya tatu (102/3)*** ya mwaka wa 2008 yameteremka kutoka alama ya wastani **43.49** mwaka wa 2007 hadi **31.17** mwaka wa 2008.
- 4.1.4 Kushuka kwa karatasi zote tatu kumeathiri vibaya matokeo ya Kiswahili kwa jumla mwaka wa 2008. Alama ya wastani ya Kiswahili ya mwaka wa 2008 imeshuka kutoka **91.51** mwaka wa 2007 hadi **74.55** mwaka wa 2008.
- 4.1.5 Alama ya tanganisho inaonyesha kuwa kuna baadhi ya watahiniwa ambao waliweza kujipatia alama nyingi zaidi ya alama ya wastani mwaka wa 2008. Alama hii ilikuwa **32.25**.

4.2 INSHA (102/1)

Jedwali 7: Matokeo ya Karatasi ya kwanza ya miaka ya 2005 hadi 2008.

Mwaka	2005	2006	2007	2008
Alama ya Wastani	20.25	15.31	15.80	14.20
Alama ya Tanganisho	6.37	7.68	6.42	7.18

Jedwali hili laonyesha kwamba isipokuwa mwaka wa 2005, matokeo ya karatasi ya 102/1 yamekuwa mabaya na kwamba watahiniwa wengi hawajaweza kujipatia alama zaidi ya nusu ya alama zote ambazo zinaweza kutuzwa.

Tutachanganua swali la kwanza ambalo lilikuwa la lazima na ambalo halikufanywa vizuri, na vilevile swali la tatu ambalo liliwatatiza watahiniwa.

Swali la kwanza

Insha ya lazima.

Andika tahariri kwa gazeti la *Raia* ukieleza hatua zinazochukuliwa nchini ili kumwendeleza kielimu mtoto msichana.

Watahiniwa walikosa alama kwa sababu wengi waliandika barua kwa Mhariri badala ya kuandika tahariri. Hali kadhalika, wengine hawakutimiza idadi ya maneno iliyo hitajika. Insha hii ilipaswa kuandikwa ifuatayo:

- (i) Tahariri iwe na sura ifuatayo:
 - Kichwa Cha gazeti: **GAZETI LA RAIA**.
 - Tarehe chini ya Kichwa.
 - Mada, kwa mfano: “Elimu ya Mtoto-msichana.”
 - Utangulizi.
 - Mwili/maelezo kiaya.
 - Maelezo yaweza kuwa na maoni au msimamo wa mhariri au wa gazeti.
 - Hitimisho kwa mfano jina la mhariri na wadhifa wake.
 - Sahihi.
- (ii) Lugha ilenge kuwasilisha na kuzindua umma kuhusu juhudzi zile za kuhakikisha kuwa mtoto wa kike amepata elimu hadi viwango vya juu.
- (iii) Lugha pia ijikite katika uhalisi wa mambo na wala si porojo au upuzi.
- (iv) Baadhi ya hoja za kuzingatia ni:
 - Kupiga vita ndoa za mapema.
 - Kupiga marufuku ajira ya watoto.
 - Wasichana kupewa nafasi ya kuendelea na masomo baada ya kujifungua.
 - Alama za kujunga na shule na vyuo vikuu kupunguzwa kwa wasichana.
 - Elimu bila malipo kwa watoto katika shule za msingi na za upili.
 - Kutoa msaada wa karo kwa watoto kutoka familia maskini.
 - Kujenga shule zaidi za wasichana.
 - Mashirika yasiyo ya kiserikali kufadhili miradi ya elimu.
 - Kuhamasisha wazazi kuhusu umuhimu wa elimu ya mtoto wa kike.
 - Adhabu kali kwa wabakaji.
 - Washikadau wote katika elimu kuhakikisha uzingativu na uendelezaji wa sera zijengazo usawa wa kijinsia.
 - Kuondoa vikwazo vya kitamaduni kama vile ukeketaji wa wanawake.

Swali la Tatu

Matikiti na matango ndiyo maponya njaa.

Hili lilikuwa swali la methali. Watahiniwa walipotoka katika kutafsiri maana ya methali hivyo basi wakapotoka katika hoja walizoshughulikia. Aidha, watahiniwa wengi hawakulijaribu swali hili kabisa.

Majibu yaliyotarajiwa

(a) Msamiati wa methali:

- Matikiti na matango ni aina ya vyakula visivyothaminiwa sana.
- Maponya ina maana ya yanayookoa au yanayofaa.
- Njaa ina maana ya shida.
- Maana kuwa vitu tunavyodunisha/tunavyopuuza huweza kuwa vya msaada mkubwa wakati wa shida.
- Kitu tulichonacho mkononi ndicho kiwezacho kututoa taabani wakati wa shida na hivyo basi tusividharau vitu tulivyonavyo.

(b) Watahiniwa walitarajiwa kuandika kisa kinachoonyesha sehemu mbili za methali:

- i) upuuzaji/udunishaji wa mtu au kitu au jambo.
- ii) mtu, kitu au jambo lije liwe ni la manufaa baadaye wakati wa shida.

4.3 MAPENDEKEZO:

4.3.1 Walimu wazidi kuwapa wanafunzi mazoezi zaidi katika uandishi wa kiuamilifu.

4.3.2 Walimu watumie silabasi za K.I.E na K.N.E.C katika ufundishaji wao.

4.3.3 Wanafunzi wahimizwe kusoma magazeti na kujifahamisha na matukio ya kila siku katika jamii na mazingira yao-kitaifa na pia kimataifa; ilmuradi waweze kuyashughulikia maswali yanayohusu maswala ibuka iwapo yatatahiniwa. Haitoshi kujifunga katika maswala yaliyo vitabuni pekee.

4.4 LUGHA (102/2)

Jedwali 8: Matokeo ya Karatasi ya pili (102/2) ya miaka ya 2005 hadi 2008.

Mwaka	2005	2006	2007	2008
Alama ya Wastani	34.08	40.60	32.22	29.18
Alama ya Tanganisho	10.61	11.80	11.91	11.43

Matokeo ya karatasi ya 102/2 yameshuka mwaka wa 2008. Matokeo haya ndiyo ya chini zaidi katika kipindi cha miaka minne. Maswali ya ufahamu na ufupisho/muhtasari ndiyo yaliyowatatiza watahiniwa. Tutayachanganua hapa.

Swali la kwanza

UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Kuna aina kuu za hisia zinazotawala na kuongoza maisha ya mwanadamu: kuona, kusikia, kugusa, kuonja na kunusa. Ni vigumu kusema ni hisia gani muhimu kuzidi nyingine ingawa ni dhahiri athari kubwa humuangukia mahuluku asiyeweza kuona. Inasemekana kuwa mishipa ya fahamu inayounga ubongo na macho ni mikubwa zaidi kuliko mishipa ya fahamu inayounga ubongo na viwambo vya masikio. Na katika maisha na nyendo za kila siku kuona hupewa uzito mkubwa **minghairi ya kusikia**. Pengine basi sio ajabu, kama itakavyobainika punde baadaye, kuwa kazi nyingi za fasihi andishi zimeelemea mno katika hisia hii kana kwamba zile nyingine kuu hazipo kabisa. Hakika hili ni kosa. Maana kusikia, kugusa, kuonja, na kunusa nako ndiko humkamilisha mwanadamu aweze kuyafaidi maisha yake. Na hata mbele ya sheria, ushahidi huweza kutolewa mintaarafu ya kusikia, kugusa, kuonja na kunusa alimradi shahidi awe amesikia, kugusa, kuonja, au kunusa mwenyewe. Ushahidi wa kuambiwa haukubaliwi.

Kwa hivyo basi kazi ya sanaa ambayo itazituma fikira za msomaji zihisi kuona, kusikia, kuonja, kugusa, na kunusa matendo na mazingira yanayosimuliwa humpeleka msomaji huyo katika mipaka na nyanja za juu za ufahamu na furaha.

Kila hisia ina umuhimu wake kutokana na mazingira ya tukio linalohusika au kusimuliwa. Maana kazi zote za sanaa hutokana na matendo na maisha ya watu ambao katika matukio, visa na mazingira yao hutumia hisia zao zote tano ama kwa pamoja au kwa nyakati mbalimbali. Ili basi msomaji aweze kupata mandhari kamili, na hata yeche mwenyewe ashiriki katika matukio yenye kwa kuchukia, kuonea huruma, n.k., muhimu, kabla ya yote, apate hisia zote hizo tano. Kazi ya sanaa inayojihusisha na hisia moja tu au mbili huwa **muflisi kisanii** kwa vile inashindwa kuwasilisha mandhari za hali halisi kwa msomaji. Je, mara ngapi nyoyo zetu husononeka au kuripukwa kwa maya kwa sababu ya sauti ndogo tu ya ndege aliaye pekee nyikani, au nyimbo ya zamani? Sauti ya ndege huweza kuleta majonzi ya miaka mingi mno ya utotonu wakati ambapo mtu alifiwa na mzazi, ndugu, jamaa au sahibu wake. Kadhalika nyimbo ya kale huweza kuchimbua ashiki ya zamani baina ya wapenzi, au kutonesha **jeraha la masai** na madhila yaliyopita. Na wala sio nyimbo na sauti ya ndege tu, pengine hata harufu ya maua huwa na nguvu za kumbukumbu kubwa mno.

Licha ya yote hayo, matumizi ya hisia nyingi yanasaidia kujenga mandhari kamili ya tukio katika akili ya msomaji. Mathalan badala ya kuelezwu tu kuwa paliandaliwa chakula kizuri, msomaji anaelezwa vitu ambavyo vimeandalialiwa pamoja na harufu yake. Au badala ya kuambiwa mtu fulani alikuwa na wajihii wa kutisha, huelezwa na kuelewa vyema zaidi kwa kuainishia jinsi pua, macho, rangi, nywele, mdomo na meno ya mtu huyo yalivyo. Na hivyo hivyo kwa mifano mingine kadha wa kadha kama vile hasira na ucheshi. Kutokana na maelezo ya kutosha ya hisia msomaji huweza **kumuashiki janabi**, au akadondokwa na ute kutamani chakula ambacho hakipo mbele yake.

Na sio hivyo tu. Hisia zinazotumiwa huweza kumfanya msomaji atafakari zaidi. Atawea kufikia uamuzi kuhusu picha zinazochorwa kutokana na hisia mbalimbali na wala sio kauli za mkatomkato za mwandishi kama ilivyogusiwa hapo juu. Kauli za mkatomkato sio tu hudumaza sanaa, bali pia hudhalilisha hata akili ya msomaji: **kwani umbuji** wa mwandishi ni pamoja na kufanya matendo na mazingira anayoyasimulia yawasilishe na kuwakilisha fikira za wahusika wake na hata zake mwenyewe.

Hivyo ni dhahiri kuwa hisia humsaidia msomaji kuzama katika matendo na kuelewa fikra za mwandishi mwenyewe, asili na makazi yake, kuwadadisi na kuwaelewa wahusika wenyewe, n.k.

Makala kutoka:

*Saffari, A.J. ‘Hisia Katika Fasihi Andishi’
Katika Mulokozi, M.M na Mung’ong’o (Wah.)
(1993:33) **Fasihi, uandishi na uchapishaji**
Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam Univ. Press*

- (a) Taja na ueleze uwanja ambao hutilia mkazo hisia zote.
- (b) Kwa mujibu wa kifungu hiki, ni nini matokeo ya kusisitiza hisia ya kuona katika fasihi andishi?
- (c)
 - (i) Mwandishi ana maoni gani kuhusu kazi nzuri ya sanaa.
 - (ii) Maoni hayo yana umuhimu gani?

- (d) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu ulichosoma.
- (i) muflisi kisanii
 - (ii) jeraha la masaibu.....
 - (iii) kumuashiki janabi.....
 - (iv) umbuji.....

Kwa ujumla, maswali ya kifungu yalihitaji mtahiniwa asome, aelewe na kuchanganua, kusanisi, kutafsiri, kutathmini na kutumia maudhui katika kifungu kujibu maswali. Watahiniwa wengi waliinua majibu moja kwa moja kutoka kwa kifungu, jambo ambalo linafanya majibu yasiwe na mtiririko unaordhisha. Watahiniwa pia walikosa alama katika swalii hili kwa sababu wengi hawana stadi ya kujieleza vizuri na hufanya makosa mengi ya sarufi na tahajia.

Majibu

- (a)
 - Uwanja wa sheria.
 - Ushahidi waweza kutolewa mintarafu ya hisia zote. (tano)
 - Ushahidi huweza kutolewa mintarafu ya kuona, kusikia, kuguza, kuonja na kunusa.
- (b)
 - Hushindwa kukamilisha mwanadamu kuyafaidi maisha yake.
 - Haimpeleki msomaji katika mipaka na nyanja za juu, ufahanu na furaha.
 - Msomaji hatapata mandhari kamili.
- (c)
 - (i) Kazi nzuri ya sanaa ni ile inayohusisha hisia zote.(tano)
 - (ii)
 - Humkamilisha mwanadamu ili ayafaidi maisha yake.
 - Humpeleka msomaji katika miaka na nyanja za juu za ufahamu na furaha.
 - Msomaji hupata mandhari kamili.
 - Msomaji atawea kushiriki katika matukio yenye.
- (d)
 - (i) ***muflisi kisanii:*** pungufu kisanii, haffifu, isiyoweza kutosheleza kisanii, duni, yenyewe kasoro au dosari, iliyo chapwa.
 - (ii) ***jeraha la masaibu:*** matatizo, machungu, mateso, taabu, shida, dhiki n.k.
 - (iii) ***kumuashiki janabi:*** kumhamasisha, kumteka, kumfanya apende, kumtamanisha, kumfanya avutiwe, kumteka akili, kumtia hamu au shauku.
 - (iv) ***umbuji:*** ubunifu, uundaji, ufundi, utunzi, ubingwa.

Swali la pili:

UFUPISHO

Uchumi wa soko huria ni hali ya kiuchumi ambapo itokeapo amali, shughuli na harakati zote za kiuchumi ghairi ya zile ambazo ni za lazima kwa serikali au dola kama ulinzi, sheria na mpangilio mzima wa jamii, huwa huria kwa watu binafsi. Msingi wa soko huria, sifa kuu ya utandawazi, ni kuibua na kudumisha mazingira na hali zinazochochea na kumruhusu mtu yelete kuongozwa na hawaii, au matamanio ya kibashara anayoyaona sawa pasi na hofu ya kuingiliwa na udhibiti wa serikali.

Mazingira hayo yanawapa watu satua ya kufanya maamuzi kuhusu hatima yao ya kiuchumi, uamuzi kuhusu suala la ajira yao, matumizi ya mtaji – kipato na harija zake, na uwekezaji mzima. Suala mojawapo linalobuka kuhusiana na mfumo wa soko huria ni kuweka mipaka bainifu na wazi baina ya amali na shughuli zinazohusishwa na serikali na zile ambazo huachwa huria kwa watu. Kwa mfano, inaaminiwa kuwa haki ya kuishi na kulindwa dhidi ya shambulizi, liwe la kijambazi au la kigaidi, ni ya kimsingi ambayo haiwezi kuhusishwa na uwezo wa kiuchumi wa mtu binafsi. Aidha huduma za kimsingi za afya nazo zinaingia katika kumbo hili. Ikiwa huduma hizi zitaachwa huria pana uwezekano mkubwa kuwa zitaishia kuwa istihaki ya wenye mtaji na kipato cha juu tu.

Licha ya kuwepo kwa sheria au kanuni huria kutoka nyanja maalum, hutokea hali ambapo udhibiti wa kiserikali ni lazima. Hili hutokea pale ambapo ipo haja ya kuyalinda mazingira hasa kutokana na uchafuzi wa viwanda au tasnia. Aidha udhibiti huo ni lazima pale ambapo haki za watu wengine zinahusika; yaani ikiwa uhuru wa hata mtu mmoja unaadhirika kutokana na sera hizo, pana haja ya kuingilia ili kuisawazisha hali yenye.

- (a) Andika kwa muhtasari maana ya uchumi wa soko huria kulingana na taarifa hii.

(maneno 25-30)

Matayarisho

Jibu

- (b) Eleza mawazo makuu yanayojitokeza katika aya ya pili na ya tatu.

(Maneno 70-75)

Matayarisho

Jibu

Swali hili lilihitaji mtahiniwa asome kifungu na kusanisi hoja muhimu na kuzifanyia muhtsari bila kuacha mawazo muhimu wala kupoteza maana asili ya kifungu. Mtahiniwa pia alihitaji stadi ya kutumia viunganishi vifaavyo ili kuleta mtiririko unaordhisha. Watahiniwa wengi walilemewa katika upande wa kutumia viunganishi ili kutiririsha mawazo. Wengi waliinua sehemu ambazo hazikuwa na uhusiano wowote kohoja. Stadi ya kujieleza kwa mtiririko ufaao lazima ifundishwe.

Majibu

- a) Uchumi wa soko huria ni hali ya kiuchumi ambapo shughuli zote za kiuchumi ghairi ya zile ambazo ni za lazima **kwa serikali** huwa huria kwa **watu binafsi**.

(b)

- Soko huru huwawezesha watu kuamua hatima yao kiuchumi.
- Suala ibuka ni kuweka mipaka baina ya shughuli zinazohusishwa na serikali na zinazoachwa huria kwa watu binafsi.
- Haki ya kuishi na kulinda dhidi ya shambulizi haiwezi kuachiwa watu binafsi.
- Huduma hizo zikiachwa huru zitaishia kuwa istihaki ya watu wa kipato cha juu.
- Huduma za kimsingi za afya haziwezi kubinafsishwa.
- Udhibiti wa kiserikali hutokea kuyalinda mazingira dhidi ya uchafuzi.
- Pia, udhibiti huo hutokea katika kulinda haki za watu binafsi.
- Soko huru huwawezesha watu kuamua hatima yao kiuchumi.
- Suala ibuka ni kuweka mipaka baina ya shughuli zinazohusishwa na serikali na zinazoachwa huria kwa watu binafsi.
- Haki ya kuishi na kulinda dhidi ya shambulizi haiwezi kuachiwa watu binafsi.
- Huduma hizo zikiachwa huru zitaishia kuwa istihaki ya watu wa kipato cha juu.

- 4.5.1 Walimu waendelee kuwapa wanafunzi mazoezi ya maswali ya ufahamu na kusahihisha wakizingatia sarufi kwa sababu jambo hili linazingatiwa wakati wa kusahihisha mtihani wa kitaifa.
- 4.5.2 Wanafunzi wasisitiziwe kwamba baadhi ya maswali ni ya stadi za juu kama matumizi na tathmini kwa hivyo maswali ambayo hayaonekani kuwa na majibu ya kuinua moja kwa moja huulizwa pia.
- 4.5.3 Mazoezi ya muhtasari huku mtiririko ufaao ukisisitizwa lazima yapewe wanafunzi mara kwa mara ndio wazoei kutumia viunganishi kutiririsha hoja katika kujibu maswali ya muhtasari.
- 4.5.4 Masuala yote katika silabasi yafundishwe katika upana wake bila kubagua.

4.6 FASIHI (102/3)

Jedwali 9: Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya miaka ya 2005 hadi 2008.

Mwaka	2005	2006	2007	2008
Alama ya Wastani	37.57	48.48	43.49	31.17
Alama ya Tanganisho	14.01	14.63	13.12	13.64

Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2008 yameshuka sana kutoka alama ya wastani ya **43.49** mwaka wa 2007 hadi **31.17** mwaka wa 2008. Tutachanganua swali la kwanza pekee katika karatasi hii kwa sababu ndilo lililookeekana kuwapa watahiniwa changamoto kidogo. Swali la ushairi huhitaji mtahiniwa kusoma, kuelewa maudhui ya shairi, dhamira, lugha iliyotumiwa pamoja na istilahi za kifasihi zinazotumiwa.

Watahiniwa walitatizika kwa kutozielewa mbinu za kifasihi na pia kushindwa kuandika katika lugha ya nathari ambapo wengi waliinua tu mishororo ya ubeti badala ya kueleza hoja zilizokuwepo kwa lugha ya kawaida. Hali kadhalika, watahiniwa wengi walitatizika katika kulielewa shairi hasa umbo lake. Wengine walibainisha udhaifu wao katika kufahamu na kuzieleza mbinu mbalimbali za uandishi zilizotumiwa. Iling' amuliwa kwamba watahiniwa wengi hawakutarajia swali la ushairi kuwa la lazima.

(LAZIMA)

USHAIRI

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

WASAKATONGE

1. Wasakatonge na juakali

Wabeba zege ya maroshani,
Ni msukuma mikokoteni,
Pia makuli bandarini,
Ni wachimbaji wa migodini,
Lakini maisha yao chini.

2. Juakali na wasakatonge

Wao ni manamba mashambani,
Ni wachapa kazi viwandani,
Mayaya na madobi wa nyumbani,
Ni matopasi wa majaani,
Lakini bado ni masikini.

3. Wasakatonge na juakali

Wao huweka serikalini,
Wanasiasa inadarakanii,
Dola ikawa mikononi,
Wachaguliwa na ikuluni,
Lakini wachaguaji duni.

4. Juakali na wasakatonge

Wao ni wengi ulimwenguni,
Tabaka lisilo ahueni,
Siku zote wako matesoni,
Ziada ya pato hawaoni,
Lakini watakomboka lini?
(Mohammed Seif Khatib)

- (a) “Shairi hili ni la kukatisha tamaa”. Fafanua rai hii kwa kutoa mifano minne.
- (b) Taja tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi zima na uonyeshe mifano miwili ya jinsi ilivyotumika.

- (c) Eleza umbo la shairi hili.
- (d) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari.
- (e) Onyesha mifano miwili ya maadili yanayojitokeza katika shairi hili.
- (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivytumiwa katika shairi.
 - (i) Manamba
 - (ii) Tabaka lisilo ahueni

Majibu

- (a)
 - (i) Wanajamii wanajishughulisha katika kazi mbalimbali ili kuboresha maisha yao lakini maisha yao ni duni.
 - (ii) Vibarua wanaoajiriwa wanafanya kazi kwa bidii lakini mishahara yao ni duni.
 - (iii) Viongozi serikalini wamepewa nyadhifa hizo za hadhi lakini hawawajibiki kwa wale waliowachagua, hawawajibiki kunyanya hali za wale waliowachagua.
 - (iv) Tabaka la chini ndio walio wengi katika jamii na ndio tegemeo la jamii lakini wanaishi maisha ya mateso mengi.
 - (v) Haijulikani mateso ya walio wengi yatafikia kikomo lini.

(b)

(i) *Kinaya*

- Wasakatonge ndio wengi lakini hawana sauti.
- Makuli, mayaya, manamba, wachapakazi, madobi na matopasi ni maskini
- Wasakatonge wafanyao kazi kwa mateso mengi ni wenye mishahara duni.
- Wapelekao watu serikalini hawashughulikiwi na waliowachagua.
- Wazalishao mali hawana chochote bado maskini.

(ii) *Taswira*

- Wabeba zenge maroshani.
- Msukuma mikokoteni.
- Makuli bandarini.
- Manamba mashambani.
- Wachapakazi viwandani.
- Matopasi wa majaani.
- Wanasiasa madarakani.
- Mayaya na madobi wa nyumbani siku zote wako matesoni.

(iii)

Takriri

- Wasakatonye.
- Juakali.
- Lakini limetumiwa mwanzoni mwa kila mshororo wa mwisho wa ubeti (kikwamba).
- Wao.
- Ni.

(iv) ***Ulinganishi***

- Wachimbaji wa migodi lakini maisha yao chini.
- Wachapakazi viwandani lakini bado ni maskini.

(c)

- (i) Kipande kimoja.
- (ii) Shairi lina kituo, kimalizio.
- (iii) Mizani hailingani katika kila ubeti.
- (iv) Beti 4.
- (v) Mishororo 6 kwa kila ubeti (Tasdisa, usita) au kila ubeti una kishwa/kijichwa, anwani na mishororo 5.
- (vi) Katika mshororo wa kwanza vina vinabadilika – LI na NGE.
- (vii) Mishororo mitano ya mwisho ina vina vnavyofanana – NI.
- (viii) Pindu – mshororo wa kwanza unajipindapinda.

(d)

Watu wa tabaka la chini ndio huwapa nyadhifa viongozi. Kutokana na nyadhifa hizo viongozi hupata mali au uwezo wa kiuchumi (kuiongoza nchi). Wale waliowachagua maisha yao ni ya kusikitisha.

(e)

- (i) Kufanya kazi kwa bidii.
- (ii) Kuwajibika – kwa umma katika kushiriki katika kuwachagua viongozi.
- (iii) Viongozi wanatarajiwa kuadilika kwa kunyanya hali ya umma kwa kujali hali ya wafanyakazi.

(f)

- Manamba – Vibarua/wafanyikazi katika mashamba.
- Tabaka lisilo ahueni - watu maskini/wasio na hali nzuri.
- Kiuchumi/walalahoi.

4.7 MAPENDEKEZO

- 4.7.1 Ni vizuri walimu wakiendelea kuonyesha wanafunzi kwamba ushairi ni jambo la kawaida linalowekwa katika lugha ya kishairi ndio waweze kuupenda.
 - 4.7.2 Walimu wawasaide wanafunzi kuweza kutofautisha dhamira, maudhui katika ushairi na pia wasaidiwe kutambua mbinu tofauti tofauti za kifasihi katika mashairi.
 - 4.7.3 Wanafunzi waendelee kusisitiziwa kwamba kuandika katika lugha ya nathari si kuinua mishororo mizima na kuipachika vile ilivyo, bali ni kuitambua hoja muhimu katika kila mshororo na kuiandika kwa lugha ya kawaida.
 - 4.7.4 Wanafunzi wahimizwe kutambua masuala muhimu yanayojiteza katika hadithi zote katika Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine.
 - 4.7.5 Wanafunzi wawekewe misingi bora katika fasihi simulizi tangu kidato cha kwanza. Katika swali linalolenga tabia za mhusika, ni muhimu kuzingatia pande zote - nzuri na baya.
- TANB. Ni dhahiri kwamba kwa jumla matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili yamezidi kudororora; na kwa hivyo ni muhimu walimu wajitahidi kutumia mbinu zote za ufundishaji na utayarishaji wa watahiniwa kwa mitihani yao.